# BUBIDOBE COMPANY LIMITED

**PO Box 5127, Mob 0787912282**

**Dar Es Salaam**

**Kumb: Na: BIBUDOBE/ARDHI/2024/10/01**

**29 October 2024**

**Msajili wa Hati**

**Wizara ya Nyumba na maendeleo ya makazi**

**Dar Es Salaam**

Ndugu,

YAH: **KUKABIDHIWA HATI YA KIWANJA NAMBA 73 GUINEA ROAD OYSTERBAY TULIYONUNUA KWENYE MNADA TAREHE 16 SEPTEMBER 2014**

Husika na kichwa cha Habari hapo juu. Kampuni yetu ni mmliki halali wa nyumba na kiwanja tajwa hapo juu, baada ya kununua kwenye mnada ulioamriwa na mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu **tarehe 16 September 2014**, kwa kulipa bei iliyokuwa ya juu kwenye mnada huo. Nyaraka mbalimbali ikiwemo certificate of sale, na kuziwakilisha katika ofisi yenu na kulipia malipo ya uhamishaji Kiserikali.

Cha kushangaza ni kwamba ofisi yako imekataa kutukabidhi hati na hivyo kusababisha sisi wanunuzi kushindwa kuingia na kulimiliki tutakavyo. Na pia kitendo hicho yaani kunyimwa hati kumempa mmiliki wa zamani ambae ni Shirika la Posta uhalali na uzito wa kuachia eneo hilo kwa kuweka walinzi ambao wanazuia kuingia ndani hivyo kwa kipindi chote cha miaka takribani kumi na kukataa kabisa kuondoka eneo hilo bila sababu yoyote ya msingi.

Kwa barua hii tunaiomba ofisi ya Waziri wa ardhi na Makazi, na watendaji wake kusaidia katika kumaliza jambo hili kwa kutupatia hali yetu ya msingi ambayo ni hati ya umiliki na kuwajulisha Posta juu ya matokeo ya kukaidi kuridhia kutupa haki yetu.

Wako katika ujenzi wa Taifa

**BUBIDOBE COMPANY LIMITED**

M. N. Ngasani

**Mkurugenzi**

Aione;

1. Ofisi ya Rais -Ikulu
2. Waziri wa Ardhi na Nyumba na Maendeleo ya Makazi
3. Kamishna Mkuu Wizara ya Ardhi- Kwa hatua zako muhimu